BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Saba – Tarehe 21 Septemba, 2023
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa mwaka 2022/2023.

### Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2022/2023.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii Kuhusu Ripoti ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale juu ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Ripoti ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa mwaka 2022/2023.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati Kuhusu Ripoti ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini juu ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

46. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Kuzagaa kwa mifugo katika maeneo ya Meli nne Magirisi na Meli nne Bondeni imekuwa ni changamoto na kero kubwa kwa wakaazi wa maeneo hayo. Pamoja na ukweli kuwa malalamiko ya kuzagaa huko yameshafikishwa kwenye vyombo husika, bado hadi sasa tatizo hili linawakereketa na kuwasumbua wananchi.

    Je, ni ipi kauli ya Serikali juu ya kuwaondoshea wananchi hawa kadhia hii.

50. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Uwepo wa taa za mitaani unasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza wimbi la wahalifu, vibaka na wakwapuaji ndani ya jimbo la Mwanakwerekwe.

    Je, Serikali haioni kwamba ipo haja ya kuweka taa hizi za mitaani kwa maeneo hatarishi kama vile Meli Nne Bondeni, Meli Nne Njia ya Uzi, Magirisi na maeneo ya Magogoni ndani.

### Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

88. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

    Kuna wastaafu ambao wanapokelea pencheni zao kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na wako wastaafu wanaopokelea pencheni zao kutoka ZSSF kama ambavyo nyongeza kutoka kwa Mhe. Rais ilivyoeleza. Hata hivyo, wako wastaafu ambao walichangia kwa miaka zaidi ya nane na haikufikia miaka kumi.

    (a) Je, wastaafu hawa waliokumbwa na kadhia kama hii Serikali inawafikiriaje.

(b) Je, Serikali haioni kuwa iko haja ya kuiboresha Sheria ya Mfuko wa ZSSF ili kuweza kuwashirikisha wastaafu ambao hawajafikia miaka ya kiuchangiaji.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

24. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Tunaishukuru sana Serikali kwa kututengenezea njia kubwa ya Melinne Makaburini angalau kwa kiwango cha kifusi, matengenezo ambayo hufanyika mara kwa mara. Kwa kuwa njia hiyo inapotengenezwa kwa njia ya kifusi huharibika mara kwa mara na kuleta usumbufu kwa wananchi.

Je, Serikali haioni kwamba huu ni muda muafaka wa kuitengeneza kwa kiwango cha lami hasa ikizingatiwa kuwa barabara hii ni kiungo kikubwa na cha pekee kwa wanaokwenda Magogoni, Nyarugusu na Kwarara.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

86. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Tasnia ya sanaa ni moja kati ya eneo ambalo vijana wetu wengi wamejiunga nalo. Hata hivyo wasanii wengi wa hivi sasa katika utunzi wa mashairi na nyimbo zao hawatumii lugha za kificho (Tafsida). Matokeo yake maneno wanayoyatumia hayatoi taswira njema mbele ya jamii zetu.

(a) Je, ni ipi kazi ya Baraza la Sanaa, Sensa ya Elimu na Utamaduni (BASFU) kwa sasa kupitia eneo hili.

(b) Je, mashairi na nyimbo hizo huwa hazihakikiwi au kukaguliwa kabla ya kurekodiwa na kuruhusiwa kupigwa hadharani.

(c) Kama kweli zinahakikiwa na kukaguliwa, je ni kwa nini baadhi ya nyimbo zinakiuka maadili ya Mzanzibari.

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

33. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Sababu zipi za kiutafiti zinazopelekea mimea mingi ya mboga mboga za asili kama vile mchicha wa asili, mchunga, na mayugwa kutoweka na kuadimika.

Je, Wizara ina mpango gani mbadala wa kushughulikia na tatizo hili ili kulipatia ufumbuzi wake.

Wizara ya Afya:

62. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Tunashukuru Serikali kwa kutusaidia kuziimarisha huduma za afya nchini.

(a) Je, ni lini tutaondolewa pesa za kodi ya gari ya wagonjwa kutoka Hospitali ya Kivunge kwenda Hospitali ya Mnazi Mmoja.

(b) Je, kuna sababu zipi zinazoipelekea Wizara yako kuwatoza wananchi pesa za kodi ya gari ya wagonjwa, wakati gari hiyo inamilikiwa moja kwa moja na Wizara yako.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:

Ripoti ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa mwaka 2022/2023.

Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

Ripoti ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2022/2023.

Zanzibar,
21 Septemba, 2023.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.